

HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA. LGA/051/2019/2020/NCS /02

UPANGISHAJI WA JENGO LA BIASHARA VIWANJA VYA NGONGO NANENANE LINDI

Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea inakusudia kupangisha jengo la maonyesho ya kilimo lililopo eneo la Ngongo viwanja vya nanenane mkoani Lindi.

Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kukodisha jengo hilo kutuma maombi yao kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA KAZI
LGA/051/2019/2020/NCS /02	Kukodisha Jengo

Zoezi la tathimini ya waombaji litaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi ya Umma (Bidhaa, ujenzi, huduma zisizo za kiushauri na uteketezaji wa mali chakavu za Umma kwa zabuni) sheria namba 07 (2011) na kanuni zake za mwaka, 2013 – G.No 446 pamoja na maboresho ya mwaka 2016 na 2018

1. Fomu ya maombi inapatikana Ofisi ya katibu wa Bodi ya zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Nchingwea bila gharama yoyote. Fika chumba namba 20 kuanzia **Ijumaa tarehe 29 Novemba 2019 saa 2:00 asubuhi hadi Ijumaa tarehe 6 Desemba 2019 saa 9:30 jioni** isipokuwa siku za siku kuu tu.
2. Fomu ya maombi iajazwe kwa umakini na iwe na nakala mbili Nakala halisi na Kivuli (original + copies) ifungwe vizuri kwa rakili ndani ya bahasha, itumwe kwa **Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea S.L.P 291 Nachingwea. Mwisho wa kupokea mambi ni tarehe 6 Desemba , 2019 saa 8.00 mchana.**
3. Barua za maombi zitafunguliwa siku hiyo hiyo saa 8.30 mchana mbele ya waombaji wote/wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria katika hafla ya ufunguzi itakayofanyika katika ofisi ya katibu wa Bodi ya zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Nchingwea iliyopo kwenye jengo la Halmashauri sakafu ya chini chumba namba 20
4. Juu ya bahasha iandikwe **"Maombi ya kupangisha Jengo la Maonyesho ya Kilimo lililopo eneo la Ngongo viwanja vya nanenane Mkoani Lindi"** LGA/051/2019/2020/NCS /02
5. Maombi yatakayochelewa kufika kwa muda uliopangwa, sehemu ya maombi yatakayotumwa kwa njia ya electronic,

mfano fax, e: mail nk, hazitakubaliwa kufanyiwa tathimini bila kujali mazingira yeyote.

6. Halmashauri haitalazimika kugawa zabuni kwa mwombaji yeyote aliyefanyiwa tathimini na kuonekana ndiye aliyetaja kiwango cha juu au cha chini cha pesa.



Geoffrey M Nnauye

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA



WILAYA YA NACHINGWEA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA